

Airbnb Sasa Inapatikana kwa Lugha Nyingi Mara Mbili Zaidi

Airbnb ni soko la mtandaoni kubwa zaidi ulimwenguni kwa maeneo ya kipekee na halisi ya kukaa na vitu vya kufanya, inatoa malazi zaidi ya milioni 7 na shughuli 40,000 zinazofanywa kwa mikono, zote zinaendeshwa na wenyiji wakazi. Takribani wageni sita wanaingia kwenye nyumba zilizotangazwa Airbnb kila sekunde. Na shughuli hizi za kuingia zinafanyika ulimwenguni kote: Mwaka 2011, kulikuwa na majiji 12 yenye nyumba zaidi ya 1,000 zilizotangazwa Airbnb; leo, karibu majiji 1,000 yana nyumba zaidi ya 1,000 zilizotangazwa Airbnb. Vilevile, mnamo mwaka 2011 ni jiji moja tu lililowakaribisha zaidi ya wageni 100,000 kwenye nyumba zilizotangazwa Airbnb, lakini mwaka uliopita, zaidi ya majiji 300 yamekaribisha zaidi ya wageni 100,000.

Ingawa Airbnb tayari inatumika katika nchi na maeneo zaidi ya 191 ulimwenguni kote, tunafanya kazi daima ili kufanya tovuti yetu iwafikie watu wengi zaidi. Kuanzia Kialbania hadi Kizulu, tunataka kila mtu ahisi anakaribishwa kwenye Airbnb, bila kujali lugha anayozungumza.

Leo, tunaongeza maradufu idadi ya lugha ambazo zinawawezesha wenyiji na wageni kutumia Airbnb. Tovuti ya Airbnb, ambayo sasa inatumia lugha 62 kote ulimwenguni, inaweza kufikiwa na wazungumzaji wa lugha wazawa zaidi ya bilioni 4¹. Kwa lugha hizi mpya, tunajitahidi kuwapa wenyiji wengi zaidi fursa za kiuchumi, na kufanya iwe rahisi zaidi kwa wageni wengi zaidi kupata uzoefu wa kusafiri ambaeo ni wa ndani, halisi na wa kipekee.

Lugha 31 zinazopatikana kwenye Airbnb kwa sasa ni hizi:

1. Kialbania (Albania)
2. Kiarmenia (Armenia)
3. Kiazeri (Azabaijani)
4. Kibosnia (Bosnia)
5. Kibulgaria (Bulgaria)
6. Kichina cha Jadi (Mkoa Maalumu wa Hong Kong)
7. Kiingereza (Australia)
8. Kiingereza (Kanada)
9. Kiingereza (Uingereza)
10. Kiestonia (Estonia)
11. Kifaransa (Kanada)
12. Kijojia (Georgia)
13. Kihindi (India)
14. Kiayalandi (Ireland)
15. Kilatvia (Latvia)
16. Kilithuania (Lithuania)
17. Kimasedonia (Makedonia ya Kaskazini)
18. Kimalta (Malta)

¹ Ethnologue.com, Oktoba 2019. Lugha 62 za sasa za Airbnb zinajumuisha wazungumzaji wazawa zaidi ya bilioni 4. Jumla ya idadi ya wazungumzaji wazawa ambaeo tutawafikia kwa lugha 62 ni bilioni 4.3. (Bilioni 3.3 kutoka kwenye lugha 31 za sasa, pamoja na bilioni 1 kutoka kwenye lugha mpya 31 ambazo tunazindua sasa.)

19. Kimontenegro (Montenegro)
20. Kiromania (Romania)
21. Kiserbia (Serbia)
22. Kislovakia (Slovakia)
23. Kislovenia (Slovenia)
24. Kihispania (Ajentina)
25. Kihispania (Amerika ya Kusini)
26. Kiswahili (Afrika)
27. Kitagalogi (Ufilipino)
28. Kiukrainia (Ukrainia)
29. Kivietinamu (Vietnam)
30. Kihosa (Afrika Kusini)
31. Kizulu (Afrika Kusini)

Kwa wenyiji na wageni wetu wanaotumia tovuti au programu yetu ya Airbnb, Ni rahisi kubadili kwenda lugha mpya. Kwenye desktop, bonyeza [hapa](#) kuchagua lugha. Programu zetu za simu ya mkononi hutumia lugha iliyochaguliwa katika mipangilio ya kifaa. Ili kubadilisha, watumiaji wanaweza kwenda tu kwenye mipangilio ya vifaa vyao ili kubadilisha kwenda mojawapo ya lugha mpya tunazoziwerezsha sasa.